



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA LUSHOTO



*(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya)*

MKOA WA TANGA:

SimuNa:027-2977216

Telefax:027-2977217

E-mail:ded@lushotodc.go.tz

Website:www.lushotodc.go.tz

Ukijibu tafadhali nukuu:

Kumb. Na. LDC/20/19/82

18 Barabara ya Halmashauri

S.L.P. 32,

21782 Lushoto, Tanga.

TANZANIA.

20/06/2023

### TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto kupitia kibali cha ajira chenye Kumb na. FA.97/228/01"TEMP"/06 cha tarehe 06/04/2023 na Kumb.Na.FA.170/369/01"C"/15 cha tarehe 23/05/2023 kwa mamlaka iliyokasimiwa kwa mujibu wa marekebisho wa sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya Mwaka 2014 inawatangazia Wananchi wote wenye sifa za Muundo wa kazi kwa nafasi zifuatazo:-

#### **1.0 MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III – (NAFASI 20)**

##### **1.1 Mwombaji awe na sifa zifuatazo:-**

- i. Awe na Elimu ya Kidato cha Nne (IV) au Sita (VI).
- ii. Awe amehitimu mafunzo ya Astashahada/ Cheti katika moja ya fani zifuatazo: Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa Kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

##### **1.2 Kazi na Majukumu:-**

- i. Atakuwa ni Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa serikali ya Kijiji.
- ii. Kusimamia Ulinzi na Usalama wa Raia na Mali zao, kuwa Mlinzi wa Amani na msimamizi wa Utawala Bora Katika Kijiji.
- iii. Kuratibu na Kusimamia upangaji wa utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kijiji
- iv. Kuwa katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji.
- v. Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu katika Kijiji.
- vi. Kuandaa taarifa ya utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha Wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa umaskini, njaa na kuongeza uzalishaji mali.
- vii. Kusimamia , kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za Kijiji
- viii. Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya Kitaalam katika Kijiji.

##### **1.3 Ngazi ya Mshahara TGS B.**

## 2.0 MWANDISHI MWENDESHA OFISI DARAJA LA II NAFASI 3.

### 2.1 Mwombaji awe na sifa zifuatazo:-

- i. Awe na cheti cha Kidato cha Nne (Form IV) na Stashahada(Diploma) ya Uhazili au cheti cha NTA level 6 ya Uhazili.
- ii. Awe amefaulu somo la Hati Mkato ya Kiswahili na Kingereza maneno Themanini (80) kwa dakika moja.
- iii. Awe amepata mafunzo ya kompyuta toka Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali na kupata Cheti katika Program za "Word, Excel, Powerpoint,Internet, Email na Publisher".

### 2.2 Kazi na Majukumu:-

- i. Kuchapa Barua, taarifa na nyaraka za kawaida na siri.
- ii. Kupokea wageni na kuwasaili shida zao, na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikiwa.
- iii. Kutunza taarifa na kumbukumbu za matukio, miadi, wageni, tarehe za vikao,safari za mkuu wake na ratiba ya kazi zingine.
- iv. Kutafuta Majalada na Nyaraka zinazohitajika katika utekelezaji wa majukumu ya kazi.
- v. Kupokea Majalada na kusambaza kwa Maafisa walio katika Idara/Kitengo/Sehemu husika.
- vi. Kukusanya,kutunza na kuyarejesha majalada na nyaraka sehemu zinazohusika.
- vii. Kupanga dondoo na kufanya maandalizi ya vikao mbalimbali.
- viii. Kuandaa orodha ya mahitaji ya vifaa vya ofisi.

### 2.3 Ngazi ya Mshahara TGS C.

## 3.0 MASHARTI YA JUMLA KWA MWOMBAJI.

- i. Awe ni raia wa Tanzania.
- ii. Awe na umri kuanzia miaka 18 hadi 45.
- iii. Aambatishe nakala za nyaraka zifuatazo katika barua ya maombi:-
  - Cheti cha kuzaliwa.
  - Maelezo binafsi (CV) yenye anwani na namba za simu za kuaminika na majina matatu ya wadhamini.
  - Picha moja (passport size) ya hivi karibuni na jina la mhusika liandikwe nyuma ya picha hiyo..
  - Vyeti vya taaluma/shule na vyeti vya mafunzo ya vyuo.
  - Mwombaji aliyesoma nje ya nchi ahakikishe anaambatisha cheti cha ulinganifu(equivalent Certificate) kilichoidhinishwa na Mamlaka husika (TCU au NECTA)

- Kitambulisho cha Taifa (NIDA) na kwa ambaye hana kitambulisho hicho aandike namba ya NIDA kwenye maelezo binafsi (CV).

Mwisho wa kupokea maombi haya ni tarehe 27/06/2023 na barua za maombi zitumwe kwa anwani ifuatayo:-

**Mkurugenzi Mtendaji,  
18 Barabara ya Halmashauri,  
Halmashauri ya Wilaya,  
S.L.P. 32,  
21782 Lushoto, Tanga.  
TANZANIA.**

Tangazo hili pia linapatikana katika tovuti ya Halmashauri [www.lushotodc.go.tz](http://www.lushotodc.go.tz)

Imetolewa na :-



**Ikupa Harrison Mwasyoge  
MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA  
LUSHOTO.**

**MKURUGENZI MTENDAJI  
LUSHOTO**

**NAKALA:-** - Katibu,  
Ofisi ya Rais,  
Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma,  
Jengo la Utumishi (UDOM) na  
Eneo la Dkt. Asha Rose Migiro,  
S.L.P 2320,  
**DODOMA.**

- Mbao zote za matangazo,  
Halmashauri ya wilaya,  
**LUSHOTO**

**NB. TANGAZO HILI LINAFAUTA TANGAZO KUMB. NA. LDC/20/19/81 LA TAREHE  
07/06/2023 NA WANAOTAKIWA KURUDIA KUOMBA NI MWOMBAJI  
ALIYEKUA AMEOMBA NAFAZI YA KAZI YA KATIBU MAHSUSI TU.**